**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UCHILE

**JULAI, 2026**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA SUMBAWANGA**

**MKOA WA RUKWA**

**SHULE YA SEKONDARI UCHILE**

**Namba za mawasiliano:**

**Mkuu wa Shule.0755311154**

**Makamu Mkuu wa Shule.0763777991**

**Shule ya Sekondari Uchile**

**S.L.P. 582,**

**SUMBAWANGA.**

**Tarehe 30/04/2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi....................................**
**S.L.P .......................**
**..................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UCHILE HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2026** na atasoma tahasusi ya **HGK na CBG**

Shule ya Sekondari Uchile ipo umbali wa Kilometa 93 Kutoka Sumbawanga Mjini. Shule hii ipo katika mji mdogo wa **Laela.** Usafiri wa basi ni wa kila siku unapatikana katika kituo cha mabasi **Sumbawanga mjini** Nauli ni Shilingi **6000/=** ukipanda magari yanayotokea Sumbawanga mjini shuka stendi ya Laela unaweza kupanda bodaboda au bajaji hadi shuleni.
Aidha kama unatokea Mbeya kwenda Sumbawanga shuka stendi ya mabasi Laela, Shule ipo upande wa mashariki kutoka stendi ya mabasi Laela .Unaweza kupanda bodaboda au bajaji hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **..................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **.....................** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **………...**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) ziwe ndefu zenye rangi ya **DARK BLUU (1)** na **UGORO (1)**. Vitambaa vyote vinapatikana Laela Maduka ya Nguo ili kuepuka utofauti wa rangi za vitambaa.
ii. Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu yenye urefu wa kutosha kuchomekea
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama;
iv. Sare ya Michezo trucksuit rangi ya **BLUU BAHARI** na Raba
v. Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe.
vii. Sweta rangi ya kijani jeshi(Kijani iliyokolea).
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ya Dark bluu mshono wa solo mikono mifupi.
ix. Tai mbili (2),.*Moja rangi ya* ***UGORO*** *na nyingine* ***DARK BLUU***
x. .Tisheti Nyeusi yenye ufito mweupe mikononi na kwenye kora na zenye nembo ya Shule zinapatikana Shuleni kwa Tsh. 10,000/=;

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

#### A. KWA WANAFUNZI WA MCHEPUO WA (CBG)

i. Madaftari 09 counter book Quire three.
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Dissecting Kit moja,
iv. Lab Coat moja
v. Scientific Calculator
vi. Gloves 100pcs (boksi moja).
vii. Godoro la ft mbili na nusu (2.5) Mashuka Jozi 2 yenye rangi ya **BLUU/PINKI** blanket 1, foronya ya mto 1 yenye rangi ya BLUU/PINKI chandarua 1 rangi nyeupe au bluu iwe ya duara.
viii. Nguo za ndani za kutosha.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na skwiza 1.
xi. Jembe 1.
xii. Wanafunzi wote ni lazima waje na tochi.

## B. KWA WANAFUNZI WA MCHEPUO WA (HGK)

i. Madaftari 09 counter book Quire three.
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Godoro la ft mbili na nusu (2.5) Mashuka Jozi 2 yenye rangi ya **BLUU/PINKI** blanket 1, foronya ya mto 1 yenye rangi ya BLUU/PINKI chandarua 1 rangi nyeupe au bluu iwe ya duara.
iv. Nguo za ndani za kutosha.
v. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
vi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.
vii. Mopa na ndoo yake.
viii. Mfagio wa nje (chelewa) 1, jembe 1 na kwanja. 1
ix. Mwanafunzi ni lazima aje na tochi.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Michango yote ilipwe kupitia Akaunti**. Uchile secondary school .**Akaunti Namba **62110007595 NMB.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRIME MINISTER’S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**UCHILE HIGH SCHOOL**
**P.O. BOX 582**
**RUKWA-SUMBAWANGA.**
**DATE**: ……/……./ 2026

To: The Medical Officer
……………………………………………………………………………………………………..
Please examine …………………………………………………………..(Name of student) as to her fitness for pursuing further education at this school.
1. Hemoglobin ……………………………………………………………………………….
2. P.v Blooding …………………………………………………………………………....
3. (a) Blooding …………………………………………………………………………......
(b) Hearing ……………………………………………….……………………………..
4. Blood pressure …………………………………………………………………………....
5. Stool for routine examination ……………………………………………………….....
6. Urine for sugar ………………………………………………………………………......
7. Skin diseases ……………………………………………………………………………..

8. Leprosy …………………………………………………………………………………………..
9. Pulmonary tuberculosis ………………………………………………………………………….
10. Asthma ……………………………………………………………………………………
11. Epilepsy …………………………………………………………………………………..
12. Deformity …………………………………………………………………………………
13. Mental problem ………………………………………………………………………………….
14. Pregnancy test

Comment…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

**DESIGNATION.....................................**

## SHULE YA SEKONDARI UCHILE

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Mimi …………………………………………………………………. nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache.

Hivyo,nakubali kujiunga na shule ya Sekondari Uchile. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhii/heshima ya Shule ya Sekondari Uchile na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe ………………………………Sahihi ya mwanafunzi ………………………………..

Mimi Mzazi/Mlezi ……………………………………………………. Nimeshuhudia mtoto wangu ……………………………........................ Akikubali kwa hiari kujiunga na shule ya sekondari Uchile, ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea mtoto wangu naamini tutakuwa tunawasiliana katika kuhakikisha mwanafunzi anafanya vizuri katika masomo yake.

Tarehe ………………… Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………..

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ……………………

**Jina la Mkuu wa Shule NEUSTA NYANDWI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama**

**walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule. 0755311154**
- **Makamu Mkuu wa Shule. 0763777991**
- **Mwandamizi Taaluma. 0755521560**